**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

---

## UCHAGUZI WA SPIKA

---

**Taarifa kwa umma kuhusu kukamilika kwa zoezi la uteuzi wa wagombea wa nafasi ya Spika**

1.0 Zoezi la Uteuzi wa Wagombea wa Uchaguzi wa Spika limekamilika tarehe 10 Novemba, 2025 saa 10:00 Alasiri. Napenda kuchukua nafasi hii kuwafahamisha yale yaliyotokana na zoezi hili na mchakato mzima toka tulipoanza, tulipo na tunapoelekea.

2.0 Uchaguzi wa Spika unafanywa kwa mujibu wa Ibara ya 86 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kanuni ya 9 na Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

3.0 Ili kukidhi matwaka hayo, tarehe 4 Novemba, 2025 nilitoa Tangazo namba 14824A katika Gazeti la Serikali Toleo Maalum Namba 11 kuvijulisha vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu vinavyokusudia kusimamisha mgombea katika uchaguzi huo kufanya Mchakato na kuwasilisha jina la mgombea husika ofisini kwa Katibu wa Bunge Dodoma kabla ya saa 10.00 jioni ya tarehe 10 Novemba, 2025 ambayo ndio siku ya uteuzi.

4.0 Hadi kufikia saa 10:00 Alasiri leo tarehe 10 Novemba, 2025 Wagombea waliowasilishwa na Vyama vyao ni kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mussa Azzan Zungu kutoka Chama cha Mapinduzi (CCM);

(b) Ndg. Veronica Charles Tyeah kutoka Chama cha *National Reconstruction Alliance* (NRA);

(c) Ndg. Anitha Alfan Mgaya kutoka Chama cha *National League for Democracy* (NLD);

(d) Ndg. Chrisant Nyakitita kutoka Chama cha *Democratic Party* (DP);

(e) Ndg. Ndonge Said Ndonge kutoka Chama cha *Alliance for Africa Farms Party* (AAFP); na

(f) Ndg. Amin Alfred Yango kutoka Chama cha *Alliance for Democratic Change* (ADC).

5.0 Baada ya uchambuzi uliozingatia nafasi ya Kiti cha Spika, sifa za wagombea waliopendekezwa na vyama na matakwa mengine ya Kisheria na Kikanuni nimeridhika kwamba Wagombea wote wametimiza masharti ya Kanuni za Uchaguzi. Hivyo, nimewaidhinisha wagombea hao sita waliowasilishwa kwangu.

6.0 Hivyo, bila kuathiri Shughuli nyingine zitakazopangwa na Bunge, tarehe 11 Novemba, 2025 saa Tatu asubuhi au muda mfupi baada ya hapo, nitawasilisha majina ya Wagombea walioteuliwa kwa Wapiga kura ambao ni Wabunge Wateule wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili Uchaguzi ufanyike kwa mujibu wa utaratibu utakaotolewa wakati wa Uchaguzi.

7.0 Napenda kutoa shukrani kwa Vyama vya Siasa vinavyohusika na Wagombea wote kwa ushirikiano mlionipa katika kukamilisha zoezi la Uteuzi.

Baraka I. Leonard

**KATIBU WA BUNGE NA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**

10 Novemba, 2025